# Kilimo cha kiekolojia cha Wakulima Wadogo Hufanikisha Haki za Mazingira



# Kilimo cha kiekolojia cha Wakulima Wadogo Hufanikisha Haki za Mazingira

*Kiongozi hiki kimeandaliwa kikiwa ni sehemu ya mradi wa Kuendeleza utetezi wa ulinzi wa hali ya hewa kwa ajili ya manufaa ya wakulima wadogo katika ukanda wa Kusini na Mashariki mwa Afrika uliobuniwa na kutekelezwa kwa kushirikiana na Afrika Kontakt na La Via Campesina kwa upande wa ukanda wa Kusini na Mashariki mwa Afrika (LVC – SEAF), pamoja na michango kutoka kwa marafiki.*





*La Via Campesina na Afrika Kontakt tunakiri kuwa tuko nyuma sana katika kukabiliana na tatizo linalotukabili la mabadiliko ya tabianchi. Sehemu kubwa ya tatizo bado haijatatuliwa, ambayo ni mifumo yetu ya kiulimwengu ya masuala ya kijamii na kiuchumi inayosababisha mabadiliko ya tabianchi. Kwahiyo, lazima tupambane kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inabadilishwa. Zaidi ya hapo, tunatakiwa kushiriki katika mchakato mzima wa kutafuta njia na mikakati mbadala ya kuleta mabadiliko halisi. Wakati wa mkutano wa Mazingira wa Paris yaani COP21, wanaharakati wa masuala ya tabianchi walikuwa wakipaza sauti zao kuhusu mabadiliko ya mfumo, na siyo mabadiliko ya tabianchi. Wengi wa wanaharakati hao hapo awali walikuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Wanaharakati hao huliona suala la mabadiliko ya tabianchi kama jambo halisi na ambalo hutokea kila siku. Kwa mujibu wa maelezo yao, hatutakiwi kuwasubiri wanasiasa kuchukua hatua, na badala yake wamekuwa wakichukua hatua ambazo kwa bahati mbaya zimekuwa zikipuuzwa na wanasiasa wengi na watunga sera au wamekuwa wakidharauliwa na mfumo.*

*Lengo la kitabu hiki cha mwongozo ni kuonyesha athari za mabadiliko ya tabianchi zinazowakabili wakulima wadogo, lakini pia kugusia suluhisho ambazo wanaweza kuzitumia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.  Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia maarifa ya wakulima wadogo kutoka Uganda, Tanzania, Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya,  na Msumbiji. Kutokana na ukweli kuwa jamii za zilizoko katika nchi hizo wanategemea sana mazingira asilia na maliasili zake, wamekuwa wahanga wakubwa wa athari za mabadiliko ya tabianchi. Lakini uhusiano wao wa karibu na mazingira umewesha uwepo wa maarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine ambayo yanatumika kukabiliana na janga la mabadiliko ya tabianchi. Hali iliyopo sasa kwenye majadiliano ya kimataifa kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na madhara makubwa ya mabadiliko ya tabianchi vinahitaji kuchukuliwa hatua za dharura. Kwa sasa tunaelewa fika kuwa mfumo wa uzalishaji uliosababisha mabadiliko ya tabianchi hauwezi kutumika kukabiliana na tatizo ambalo wenyewe ulisababisha.  Badala yake tunatakiwa kufungua macho yetu ili tuweze kutambua njia zilizopo na tuweze kuziendeleza na kuzitanua ili zisaidie katika mapambano. Hili linajumuisha mabadiliko kwenye mfumo wa uzalishaji wa dunia nzima.*

# Faharasa

**Mabadiliko ya Tabianchi:** Ni mabadiliko ya muda mrefu ya hali ya hewa ya Dunia yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu, ambapo kwa ujumla husababisha kuongezeka kwa wastani wa joto duniani na kuzidi kwa hali ya kutotabirika ya mifumo ya hali ya hewa.

**Mashirika:** Haya ni makampuni yanayolenga kupata faida za kifedha (au njia nyingine), mara nyingi faida hiyo ni kwa njia ya kuuza bidhaa bila kuangalia madhara ya biashara zao kwa mazingira na watu. Katika muktadha wa kitabu hiki cha mwongozo, mashirika yanayozungumzwa ni yale yenye biashara za kimataifa (TNCs).

**Uzalishaji uliokithiri:** Ni aina ya uzalishaji unaofanywa kwenye uso wa dunia unaozingatia kuwa dunia ni kama mama kwa kila kiumbe, na siyo kama kitu chenye uhai, lakini kama rasilimali (yenye thamani) ambayo inaweza kutumika na kuzalisha faida. Historia ya mtazamo huu wa uzalishaji imetokana na watu kukiuka kwa kiasi kikubwa haki za binadamu za maeneo husika na nchi kwa ujumla, na ukiukwaji huo wa haki za biandamu ndio sababu kubwa ya uharibifu wa mfumo wa ekolojia na uasilia kwa ujumla, kwasababu mambo hayo yanaonekanakuwa si ya muhimu kuliko faida ambayo mtu anaielekeza kwenye mtaji wake.

**Mfumo dume:** Ni mfumo ambao unawakandamiza, kuwanyonya na kuwafanya wanawake kama bidhaa (miili yao, maisha na jinsi yao), na kazi wanazofanya wanawake (rasmi na zisizo rasmi, aina ya kazi na mazingira ya kazi); na ni mfumo unaowanyima wanawake hakia ya kufurahia vitu vizuri vilivyopo (rasilimali, maji, ardhi, uhifadhi wa mazingira, na uhuru wa chakula). Mfumo dume umejikita sana katika tamaduni na mila na desturi, ambazo zimekuwa zikitumika kama kisingizio cha kuendeleza mabavu na utawala dhidi ya mwanamke.

**Suluhisho potofu:** Hizi ni programu na sera zinazopigiwa upatu na mashirika, makampuni ya kilimo na serikali kama suluhisho la mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, suluhisho hizi zinatumia mbinu zilezile za kibepari ambazo zimesababisha kuwepo kwa mabadiliko ya tabianchi. Suluhisho hizi ni pamoja na kugeuza biashara, GMO, na mifuko kwa ajili ya kilimo cha kudhibiti hewa ya ukaa, na mengine. Suluhisho kama hizo, zimekuwa zikipigiwa kampeni na mashirika shawishi kwa malengo ya masoko, biashara na unyonyaji.

**Hewa za ukaa:** Hii ndo sababu kuu ya mabadiliko ya tabianchi. Zipo hewa zinazoenda kuharibu anga ambazo hutokana na moshi wa nishati ya mafuta kwenye viwanda na kwenye usafirishaji, nyingine zinatokana na uharibifu wa udongo, na matumizi ya ardhi kubadilisha uwezo wa kuhifadhi joto la ardhini na hivyo kubadilisha hali ya tabianchi.

**GMO (kiumbe kilichobadilishwa vinasaba):** GMO inamaanisha kiumbe ambacho vinasaba vyake vimebadilishwa na kuwekwa vinasaba vingine vinavyohitajika kwa malengo fulani. Katika kilimo, hii hufanyika zaidi kwa kubadilisha vinasaba vya mimea ili iweze kuhimili viuatilifu mbalimbali. Sheria za kimataifa kuhusu haki miliki zinaruhusu makampuni kuwa na miliki ya mimea iliyofanyiwa mabadiliko ya vinasaba, na kudhibiti usambazaji wa mbegu zake.

**Biashara ya kilimo:** Ni aina ya shirika au kampuni linalozalisha chakula au mazao ya kilimo (mazao ya kutengenezea mafuta, nguo nk) kwa ajili ya kupata faida, hasa hasa ni biashara inayolenga faida kwenye masoko ya kimataifa. Katika muktadha wa mwongozo huu biashara ya kilimo tunalenga kumaanisha biadhaa zote ambazo zimezalishwa kwa kutumia njia za kisasa, kwa mitambo, kilimo cha kiviwanda yaani cha mashamba makubwa, na kinachotegemea sana mbolea za viwandani na viuatilifu, na kuchakatwa viwandani na baadaye kusambazwa katika masoko mbalimbali duniani.



**Kugeuza biashara (neno lisilo rasmi – kubiasharisha):** Kugeuza biashara ni hali ya kubadilisha bidhaa, huduma, mawazo na hata watu kuwa biashara (kuuza na kununua), vinakuwa bidhaa. Siku hizi mambo mengi ambayo hayakutegemewa kufanya vyanzo vya mapato sasa hivi vitu hivyo vimegeuzwa kuwa bidhaa kama vile maji, misitu, na hewa.

**Uhuru wa Chakula:** Hii dhana ya mfumo wa chakula inayoheshimu haki za wazalishaji wa chakula kuzalisha na kuuza chakula kinacholimwa kwa mazingira ya kiutamaduni, pamoja na walaji kuwa na haki ya kuamua wanachotaka kula, na kujua kimezalishwa kwa namna gani na naniz kazalisha. Ni dhana inayozuia ushawishi wa makampuni makubwa yanayolenga kupata faida kujiingiza katika uzalishaji wa chakula. Uhuru wa chakula unahusu mabadiliko ya kimfumo – kuhusu watu kuwa na demokrasia na udhibiti wa masuala muhimu yanayohusu jamii zao – jinsi tunavyopata chakula na kujilisha wenyewe, namna tunavyotumia ardhi, maji na maliasili zinazotuzunguka kwa manufaa ya kizazi cha leo na kizazi kijacho, na jinsi tunavyohusiana sisi kwa sisi kwenye makundi yetu, kati ya watu na watu, na tamaduni mbalimbali.

# Madhara ya Mabadiliko ya Tabianchi ni dhahiri

Neno mabadiliko ya tabianchi humaanisha mabadiliko ya muda mrefu ya hali ya hewa yaliyoanza kujitokeza kuanzia karne ya 20. Yanasababishwa na hewa ya ukaa pamoja na uharibifu wa hali ya asili unaopunguza uwezo wa mazingira kufyonza hewa ya ukaa kutoka angani. Hali hii husababisha mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri mzunguko wa majira duniani kama vile majira ya mvua, kuwepo kwa majanga ya asili kama vile mafuriko yanayoleta maafa, vimbunga na ukame.

Mabadiliko ya Tabianchi tayari yameendelea kuleta madhara makubwa. Wakati athari za mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yakimkumba kila mmoja bila kujali mipaka ya nchi, wale waliosababisha mabadiliko hayo ya tabianchi hawaonyeshi kuwajibika kubeba mzigo wa athari hizo. Kiukweli, mabadiliko ya tabianchi yanaathiri, na yataendelea kuathiri, watu ambao hawakusababisha mabadiliko hayo. Ingawa mijadala kuhusu mabadiliko ya tabianchi katika ngazi za kimataifa imekuwa ikijielekeza katika makadirio ya hali itakavyokuwa siku za mbeleni na kitisho cha hali itakavyokuwa endapo hatua za kukabiliana nayo hazitafanyika, lakini ukweli uliopo ni athari hizo tayari zipo na watu wanaziona, hasa kwa watu wanaoishi vijijini walioko kusini mwa dunia. Makundi ya watu yaliyo hatarini na waliotengwa; yaani wakulima wadogo, wanawake wa vijijini, watu wasio na ardhi, na jamii asilia, hukabiliana na athari hizo za mabadiliko ya tabianchi kila siku. Mabadiliko ya mfumo wa mvua, kuongezeka kwa mawimbi ya joto, kuongezeka kwa mafuriko, na uwepo wa ukame mkali na wa muda mrefu vimewaathiri sana wale wanaotegemea ardhi kwa ajili ya ustawi wa maisha yao na hali hii ilionekana wakati wote tulipokuwa tunatembelea maeneo mbalimbali wakati wa kuandaa mwongozo huu.



Eneo la kusini mwa jangwa la Sahara liko hatarini zaidi kuathirika na

mabadiliko ya tabianchi ambapo kwa miaka mingi mfululizo kumekuwepo na upungufu wa mvua na hali ya hewa isiyotabirika ambayo imeathiri upatikanaji wa chakula na maji. Umoja wa Mataifa ulitangaza janga la njaa kwa nchi kadhaa zikiwemo Somalia, Sudani, Burundi na Ethiopia huku majanga ya mafuriko ya mafuriko yamekuwa yakiziathiri sana nchi za Msumbiji, Malawi na Zimbabwe. Zaidi ya hayo, hali halisi ya tabianchi na tafiti zilizofanyika zinaonyesha kuwa hali ya joto kwa upande wa kusini mwa Afrika itaongezeka mara moja na nusu zaidi ya wastani wa dunia kwa miaka ijayo, na hivyo kutoa picha ya giza nene kwa siku zijazo kwa ukanda huu endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa kukabili hali hii.

Faida itokanayo na viwanda kwa sehemu kubwa huchangia mabadiliko ya tabianchi. Hali inayoendelea duniani kuhusu mfumo wa uzalishaji na tabia ya kupenda matumizi hutegemea sana mafuta kutoka ardhini, nishati hii inatoa hewa ya ukaa na hivyo kuhatarisha zaidi hali ya anga. Maendeleo yanayofuata mfumo wa kiliberali, wenye lengo la kuzalisha faida kiuchumi, ukuaji usio na kikomo, na upanuzi





wa masoko, ni sababu kuu za mabadiliko ya tabianchi.

Watu wengi wanakabiliana na madhara makubwa ya mabadiliko ya tabianchi. Wakati huo huo, wale waliosababisha matatizo hayo wameendelea kuwa na mamlaka na ushawishi duniani. Mashirika makubwa yamebadilisha aina ya ushawishi wao kwenye masuala yanayohusu sera za kiulimwengu, na kusukuma mbele ajenda ya kubadilisha mifumo ya kisheria kwa ngazi za kitaifa na kimataifa kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi, na wakati huo huo wakikwamisha jitihada yoyote inayofanyika ya kupunguza ongezeko la joto kwenye sayari yetu.

## Kwanini tunahitaji kuwa na Haki ya Mazingira?



Kiukweli, Haki ya Mazingira inayolenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni vita ya kiufundi na kisayansi. Mabadiliko ya tabianchi ni matokeo ya kuwa na ubovu katika mfumo uliopo, na hatimaye mabadiliko yataweza kupatikana kwa kubadilisha mfumo uliopo. Haki ya Mazingira ni mapambano ya kuhakikisha kuwa mfumo wa uzalishaji duniani unabadilishwa na kunakuwepo na mgawanyo mpya wa rasilimali. Ni mapambano dhidi ya matabaka ya mamlaka ya mashirika, ambayo mbali na kusababisha janga hili, yamepewa jukumu la kutatua janga hilo.

Kama kichocheo muhimu cha mabadiliko ya tabianchi, uzalishaji wa chakula wa kiwango cha kiviwanda haukwepi lawama hizo. Uzalishaji mkubwa wa chakula umetawaliwa na mashirika makubwa ambayo yanafanya kazi kwa mwavuli wa uzalishaji wa kilimo cha kibiashara, ni uzalishaji unaohitaji maeneo makubwa ya ardhi, mbegu, na mfumo mzima wa chakula. Wazalishaji hao hulenga zaidi kupata faida kwa kuwapora wakulima wadogo mashamba, na mfumo wa kilimo unaoteketeza misitu na unatumia kiwango kikubwa cha nishati. Wanatumia mamlaka yao kushawishi sera

za kitaifa na kimataifa, zikiwemo sera zinazohusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, matokeo yake ni kuwa wanatoa mbinu potofu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kama vile Kilimo cha Kimazingira (Climate Smart Agriculture – CSA), Mkuhumi (REDD/REDD+), Blue Carbon nk.

Ni vema sasa mamlaka wakapewa wakulima wadogo wachapa kazi na wenye uwezo wa kuilisha dunia. Kilimo cha kibiashara kilichojikita katika nadharia ya ukuaji wa kiuchumi bila ya kujali madhara yake hakitaweza kutatua tatizo lililopo. Ulimwengu unahitaji mabadiliko ya kimfumo ambapo tutaweza kubadilisha njia zetu za kiuchumi, na kuleta mapinduzi ya mfumo wa uzalishaji chakula utakaolinda mazingira na kutoa uhakika wa chakula kwa jamii.



*Kisanduku cha 1: Mashirika Shawishi*

**L"Mashirika shawishi" ina maana ya mashirika yote yenye utajiri mkubwa ulioelekezwa katika kumiliki sehemu kubwa masoko ya kidunia kama vile masoko ya mbegu za kisasa na mbolea. Lengo lao kubwa ni kukua na kuongeza uwezo wao kumiliki uchumi. Kwahiyo, masuala yote yanayohusu madhara kwa jamii au kwa mazingira asilia si jambo la msingi kwao. Kwa kuwa wana mali nyingi wana uwezo wa kushawishi maamuzi ya kisiasa, kwa vile mashirika hayo yana utajiri katika sehemu kubwa ya dunia hii wamekuwa na ushawishi mkubwa katika maamuzi mengin duniani hasa kwenye mikutano mikubwa ya mazingira kama vile Mkutano wa Mazingira wa Paris (COP[1]), G8(20[2]), EU[3] na SADC[4]. Wanatumia**

[1] La Conférence des partis
[2] Le groupe des 8/20
[3] L'Union Européenne
[4] La Communauté de Développement de l'Afrique Australe

**ushawishi huo katika utungaji wa sera zinazowanufaisha wao pekee yao, na siyo maslahi ya jamii kwa ujumla.**

**Wanafanya hivyo si kwasababu wamechaguliwa kidemokrasia kufanya kazi za ushawishi walizo nazo na hawawajibiki kwa yeyote zaidi ya wadau wao. Mashirika kama vile Monsanto, Agrium, Bayer, Yara, Cargill, Mosaic, ChemChina na DowDupont, kwa kutaja baadhi, yamekuwa na hisa kubwa kwenye masoko ya biashara ya kilimo na wanatumia fursa hiyo kujilimbikizia faida zao – mara nyingi kwa kuhatarisha tabianchi na wakulima wadogo.**

**Mbali na kuwa mashirika haya shawishi, kwa kutojali kwao, kutowajibika kwao na kujiona wako sahihi muda wote, yamekuwa sababu kuu ya mabadiliko ya tabianchi, lakini yenyewe yamekuwa hayaonji adha ya mabadiliko ya tabianchi. Badala yake wamekuwa wakikaribishwa kwenye meza ya maamuzi na kushiriki katika kuandaa sheria ambazo zilitakiwa kutumika kuthibiti mwenendo wa biashara zao. Kwa sasa, wakulima wadogo (pamoja na wafanyakazi wa mashambani, watu wasio na ardhi, wafugaji na wavuvi), pamoja na watumiaji wa bidhaa wanaoondolewa kwenye maeneo yao au wanaoshawishiwa (kulazimishwa) kufanya kazi na kukubaliana na mfumo wa uzalishaji wa kiviwanda na kutumia vilivyozalishwa, wameachwa wakiwa waathiriwa wa madhara ya mabadiliko ya tabianchi na wananyimwa nafasi ya kushiriki katika kufanya maamuzi.**



Sehemu kubwa ya mafanikio yanayotakiwa kuwepo kupitia Haki ya Mazingira ni kukabiliana na ukosefu wa usawa katika mfumo wa uzalishaji wa chakula. Katika harakati hizi, kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kimebainishwa kuwa ndio mfumo sahihi wa uzalishaji chakula, uliojikita katika mshikamano na jamii au miongoni

mwa jamii zilizoathirika ambazo sauti zao zinanyamazishwa kwenye mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na watu wenye nguvu, ni mfumo unaowawezesha akina mama wanaofanya kazi za kilimo kuzilisha jamii zao huku wanaume wakifanya shughuli nyingine za kuongeza kipato. Wanawake hawa wakulima wadogo na wanaume wako mstari wa mbele katika vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, na kila siku hutafuta njia za kukabiliana na tatizo hilo. Tafiti nyingi huru zinazoonyesha kuwa suluhisho zinazotolewa na wakulima wadogo zinaweza kuzuia na kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi[5 6], huku wakikiendeleza kilimo na kuimarisha uhimilifu wa uzalishaji. Tunahitaji kuwa na mapinduzi ya mfumo wa chakula, ambapo nguvu, rasilimali, na uwajibikaji unakuwa katika uwiano sawa kutoka kwa mashirika shawishi kwenda kwa wazalishaji na walaji, ambao ndio wanaochangia kwa kiasi kikubwa katika mapambano dhidi ya janga la mabadiliko ya tabianchi.

## Suluhisho Potofu

Suluhisho zinazotolewa na mashirika shawishi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Wakati Mkutano wa Mazingira na mamlaka nyingine kama vile Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu Upatikanaji wa Chakula (CFS), Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), Rio+20 (UNCSD), Benki ya Dunia na mengine wakianza kuonyesha kuelewa kuhusu uhusiano ulipo kati ya kuongezeka kwa hewa ya ukaa na kilimo cha kiviwanda, majibu yake katika kutatua janga la mabadiliko ya tabianchi bado yanaakisi makosa yaliyojitokeza kwenye Mapinduzi ya Kijani (tazama Kisanduku cha 3).

Suluhisho potofu kama vile Kilimo cha Kimazingira (*Climate Smart*

[5] IFAD, 2011: *Smallholders can feed the world*. https://bit.ly/2fFO4DQ
[6] IFAD, 2013: *Smallholders, food security and the environment*. https://bit.ly/2IJ0Ko3

*Agriculture*) zinatumia kauli zinazotumika kwenye Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo, lakini kwenye kilimo cha kibiashara au cha kiviwanda[7] [8]. Hii ni pamoja na kilimo cha zao moja na mbegu zilizoboreshwa. Huku ikitumika lugha ya Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo, hakuna mahali popote katika mapendekezo hayo wanazungumzia haki za msingi na vyakula vya kienyeji, kulindwa kwa misingi ya utu, ardhi na uwezo wa kujiamulia, yaani misingi ya Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima wadogo.

Kwenye ajenda ya Kilimo cha Kimazingira, wanatumia masuala tata ya kijamii na kisiasa kwa kisingizio cha kutoa suluhisho kwa wakulima wadogo ambao "hawajandelezwa" na "wasio na elimu" kwa njia ya Mapinduzi ya Kijani. Kwa njia hii, utajiri wa wale wanaonufaika na suluhisho hizi, yaani makampuni makubwa yanayofanya biashara ya kilimo unaendelea kuwepo. Kwahiyo, haya ni Mapinduzi ya Kijani yaliyokuja kwa kifungashio kipya. Wanasema, 'kinajali mazingira', lakini kinamjali nani?



Katika muktadha huo huo, michakato ya COP[9] imepitisha suluhisho potofu nyingi zinazolinda mifumo ya masoko na kuzalisha mipango mingine ya kifedha na miundo kama vile CDM, REDD, Blue Carbon, uvunaji ma uhifadhi wa hewa ya kaboni (BECCS). Kuna uharibifu mwingi unaofanywa na kuendekezwa na wenye nguvu. Mikataba ya kimataifa isiyowalazimisha washiriki na kuondolewa kwa baadhi ya sekta za kiuchumi katika uwajibikaji, kunakwamisha jitihada za kutatua kiini cha tatizo la mabadiliko ya tabianchi, yaani kuwadhibiti mashirika shawishi na mfumo wa kiuchumi uliopo. Wao hudai kuwa suluhisho zao ambazo ni potofu kwamba zinaweza kukomesha hewa ya ukaa. Lakini kiuhalisia, njia hizi hazitoi suluhisho lolote kwa tatizo lililopo; ila badala yake zinakuza tatizo kwasababu wanaendekeza

[7] Food First, 2014: *UN-masking Climate Smart Agriculture* https://foodfirst.org/press-releases/un-masking-climate-smart-agriculture/
[8] JPS, 2017: *Climate Smart Agriculture: What is it good for?* http://tandfonline.com/doi/abs/10.1080/03066150.2017.1312355
[9] Conference of Parties

biashara ya hali asilia huku wakiendeleza madai ya uwongo kuwa ubinafsishaji na teknolojia za viwanda kwa ajili ya kilimo ndio njia pekee za kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Haki za Mazingira hazitoki juu kwa wenye mamlaka bali huanzia nchini.

## Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo

Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo ni aina ya maisha inayoichukulia dunia kwa heshima na kuithamini, na siyo kama kitu cha kunyonywa. Ni mfumo wa maisha unaonyesha kuwa upo uhusiano wa karibu kati ya binadamu na mazingira yanayowazunguka na hivyo mazingira hayo yasithaminishwe kwa pesa, na ni mfumo unaoelewa kuwa matumizi mabaya ya mazingira na kuyafanya chanzo cha pesa kutaangamiza watu na dunia nzima. Utamaduni wake umejengwa katika msingi wa kubadilishana mbegu, kupeana maarifa, kupanda aina tofauti za mazao na kuweka mzunguko mzuri wa virutubisho kwa ajili ya kulinda rutuba na uhai wa ardhi ya kilimo. Ni mfumo wa wakulima wadogo na hauwezi kuthaminishwa kwa pesa. Ni kwa njia hii ujuzi mpya wa kuzalisha mazao kwa namna inayoendana na tabianchi umebuniwa, na Kilimo cha Kiekolojia kimejengwa katika msingi huo. *Chakula lazima kilimwe kwa ajili ya binadamu, siyo kwa ajili ya faida.*



Wakulima wadogo wanaozingatia kilimo cha ekolojia huhimili na kupata nafuu haraka inapotokea kuna matatizo makubwa ya hali ya hewa kama vile ukame na mafuriko. Kwa kutumia ujuzi asilia, mbegu za kienyeji, na kupanda aina tofauti za mazao, wakulima wanakuwa na uhakika wa kupata chakula bora kwa ajili yao na familia zao. Kwa kupata nafaka zinazoweza kuhifadhiwa kwa miaka mingi kama vile mtama, ulezi, uwele, inakuwa rahisi kwa mazao hayo kuhimili ukame. Kwa kuzingatia bayoanuwai, wakulima wanalinda udongo, wanatunza nyasi na miti inayotunza maji. Kwa kutumia mbolea inayotengenezwa shambani, wakulima wadogo hutunza virutubisho



16

na kuendeleza uhifadhi wa rutuba. Si hayo tu, bali pia kitendo cha kuzalisha kwa njia ya kienyeji badala ya kuzalisha kwa lengo la masoko ya kimataifa, wanatumia nishati kidogo na hivyo kuwa na kutoa hewa kidogo ya ukaa (kwa njia ya usafirishaji na ufungashaji wa mazao kwa ajili ya kupelekwa sokoni), na hivyo kufanikiwa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Uzalishaji wa chakula kwa ajili ya kuuza nje huondoa rutuba ya ardhi kwa njia ya matumizi ya mbolea za kiwandani na viuatilifu ambavyo huharibu udongo na kuwafanya wakulima wawe watumwa wa kununua pembejeo hizo kutoka kwa makampuni makubwa ya pembejeo za kilimo. Ni kwa njia hii, makampuni makubwa ya kilimo, yakiwa sehemu ya mfumo mzima wa chakula wa dunia nzima, husababisha mahitaji ya pembejeo zao, na kuwafanya wakulima wadogo waendelee kuingia gharama za kilimo. Lakini wakulima wadogo lazima walime kwa ajili ya kupata vyakula vyenye lishe bora na siyo kutengeneza mzunguko wa utegemezi.

Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo hakipingani na teknolojia mpya. Kwa kweli, mkabala wa kilimo cha kiekolojia kinajikita katika sayansi, na kinatoa jukwaa mahususi kwa ajili ya maendeleo na kuhusisha teknolojia zenye tija. Lakini kilimo hiki kinapingana na teknolojia zinazotumika na mashirika shawishi kwa ajili ya kujimilikisha njia za uzalishaji wa chakula, ambazo zinakiuka uhuru na haki za wazalishaji na walaji, kwa maslahi ya kujipatia binafsi, lakini endapo teknolojia hizi zitachangia katika kutetea uhuru wa wakulima wadogo na uzalishaji wao, maeneo yao, utamaduni wao, na maisha yao, na kama inapigania haki za mazingira, na hivyo itaweza kuboresha maisha ya mkulima mdogo.

Kilimo cha Kiekolojia cha wakulima wadogo, na misingi ya ujuzi wa kilimo hicho, ni mfumo unaonyesha kuwa upo uhusiano wa karibu na jamii na muunganiko wa kina na ardhi na ekolojia ya maeneo husika. Kilimo hiki kimeanza kutoa matokeo mazuri katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, mafanikio yanakwamishwa na mfumo uliopo unaosisitiza mahitaji ya kupata faida inayotokana na kilimo cha mazao ya chakula.

*Kisanduku cha 2: Mzunguko wa utegemezi*

**Kilimo kikubwa cha kibiashara kina nguvu ya kuzishawishi serikali na jamii za wakulima wadogo katika kuwekeza katika uzalishaji wa mazao yao, kama vile mbolea, viuatilifu, na mbegu bora. Wanauza vitu hivyo kama njia ya kuwawezesha kuzalisha zaidi na kuwa na mazao yenye ubora zaidi.**

**Hizi ni suluhisho potofu. Wakulima wanapokubaliana na suluhisho hizi wanakuwa tegemezi kwa makampuni makubwa ya biashara za kilimo, wananaswa kwenye mtego wa kupoteza ujuzi wao wa asili na wa kitamaduni wa kuhifadhi udongo, kuhifadhi bayoanuwai na kuzalisha mbegu zao wenyewe, kutaja baadhi. Kwa njia hii masharika hayo yanatengeneza utegemezi wa wakulima wadogo na hatimaye kujipatia faida huku wakulima wadogo wanakuwa wahanga.**



**Wakishanaswa katika mzunguko huu, jamii inapoteza hazina yake ya maarifa ya asili ya kuzalisha mazao ya chakula katika hali endelevu na himilifu. Hii inakwamisha uwezo wa wakulima wadogo kutumia njia hizo katika kuboresha mfumo na kuikoa dunia.**

**Utegemezi huu huanzishwa na kuendelezwa kwa njia mbalimbali:**

> *Mbegu zinazozalishwa na mashirika haya huwa haziwezi kutumika zaidi ya msimu mmoja, hii inamaanisha kuwa wazalishaji wanatakiwa kuzinunua kila mwaka. Matumizi ya mbegu hizi huwafanya wakulima kuwa katika mahusiano ya utegemezi kwa wazalishaji wakubwa wa mbegu.*
>
> *Utegemezi wa mbolea za viwandani hupunguza uwezo wa ardhi kujitengenezea rutuba. Baada ya misimu kadhaa udongo unapoteza nguvu, na wakulima hawataweza kuzalisha mazao bila ya kutegemea pembejeo za viwandani.*

*Kuna programu zinazowahimiza wazalishaji kuchukua mikopo ili waweze kuzipata pembejeo hizi zinazozalishwa na makampuni makubwa. Mwishowe, hali hii huwafanya wakuliwa wawe na madeni, kuwa na uzalishaji duni, na ikitokea msimu wa kilimo umekuwa mbaya tofauti na walivyotarajia (kutokana na mabadiliko ya tabianchi), wakulima wadogo wanapata mavuno kidogo na hawawezi kulipa deni hilo.*




**Kilimo cha Kiekolojia ni nyenzo muhimu inayowawezesha kujinasua katika mzunguko huo wa utegemezi, kwa kurejesha udongo ulioharibika na kuimarisha uhuru wa chakula (ikiwemo uhuru wa kujiandalia mbegu) kwa jamii za wakulima wadogo, na kuhakikisha kuwa maeneo husika yanazalisha chakula na kuimarisha maisha ya watu kwa ujumla.**

# Biashara ya kilimo: Kuanzisha na kuendeleza migogoro

Kukiokoa kilimo kutoka kwenye nguvu ya soko la dunia na mashirika makubwa yanayohodhi shughuli za kilimo ndio msingi wa mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Matumizi makubwa ya nishati kwenye kilimo cha kiviwanda kinachotokana na teknolojia za Mapinduzi ya Kijani husababisha kwa kiwango kiwango uzalishaji wa hewa ya ukaa ambayo ni chanzo kikubwa cha mabadiliko ya tabianchi. Sababu ya pili ya ya janga hili ni matumizi ya ardhi. Hilo huharibu mazingira ya bayoanuwai kwa kuwa na mashamba makubwa yanayozalisha zao moja, jambo ambalo hupunguza uwezo wa dunia wa kunyonya hewa ya kaboni kutoka hewani. Kwa kuzingatia hilo, tunatakiwa kulikabili tatizo la kufanya kilimo kiwe cha kibiashara.



*Kisanduku cha 3: Teknolojia za Mapinduzi ya Kijani. Picha ya tatizo zima*

**Mapinduzi ya Kijani ni neno linalotumika kuelezea muundo wa uzalishaji unaotegemea teknolojia na shughuli za kilimo cha kiviwanda. Teknolojia zinahitaji nishati kubwa na hulenga kuongeza uzalishaji wa kilimo. Hilo huhusisha mitambo mikubwa ya kilimo, mbolea za kemikali, na mazao yaliyobadilishwa viini tete, pamoja na mambo mengine.**

**Nguvu kazi imechukuliwa na matumizi ya mitambo ya kilimo. Kwahiyo sasa hivi wanahitaji watu wachache, lakini kiwango kikubwa cha nishati ya mafuta kinatumika, na hivyo kusababisha kiwango kikubwa cha hewa ya kaboni dayoksaidi kwenda angani. Matumizi ya mbolea za viwandani**

husababisha hewa ya Naitrojeni oksaidi kuongezeka angani lakini pia huharibu udongo, na kuwafanya wakulima wadogo kuwa tegemezi kwa kununua mbolea za kemikali kila mwaka. Teknolojia hizi hufaa zaidi mashamba makubwa yanayohitaji ardhi kubwa, na hivyo hilo husababisha maeneo makubwa ya misitu kusafishwa kwa ajili ya kugeuza mashamba na hivyo kusababisha hewa zaidi ya kaboni dayoksaidi kwenda angani.

Madhara haya yamesababishwa na Mapinduzi ya viwanda ambapo hilo limesababisha shughuli za kilimo kubadilika kutoka kuwa kilimo cha kutumia mbinu za kiasili hadi kutumia teknolojia za viwanda. Mifumo hii ya kisasa ya uzalishaji hutumia nishati kubwa zaidi kuliko kilimo cha kiekolojia cha wakulima wadogo. Kiukweli, mfumo huu wa uzalishaji hauwezekani bila ya matumizi ya nishati rahisi na iliyo rahisi kutumika. Utegemezi huu ni wa msingi. Ndiyo maana jitihada za kubadilisha mfumo (suluhisho potofu) hazitaweza kupunguza hewa ili kuzuia mabadiliko ya tabianchi.



Mazao yaliyobadilishwa vinasaba pamoja na mbegu mchanganyiko ni teknolojia mpya za Mapinduzi ya Kijani zinazoonyeshwa kama njia ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuweza kuulisha ulimwengu, lakini huwadhuru wakulima na maisha yao kwa ujumla. Mbegu hizi zinatengenezwa na kumilikiwa na makampuni makubwa kama vile Monsanto, Bayer, DowDuPont, au ChemChina; mashirika haya hutumia nguvu kubwa za kifedha pamoja na nguvu za kisiasa kuzishawishi serikali mbalimbali kutunga sheria zinazowakandamiza wakulima wadogo pamoja na mbinu zao za kilimo, kama vile kubadilishana mbegu na kutunza mbegu. Kwa njia hii, wanawalazimisha wakulima kununua mbegu za kisasa pamoja na mbolea za viwandani na viuatilifu ambavyo vimeandaliwa kutumika pamoja na mbegu hizo. Programu za serikai huhimiza wakulima kuchukua mikopo ili waweze kununua kemikali hizi zinazoharibu rutuba ya udongo na mbegu zilizobadilishwa vinasaba[10].

**Baadhi ya kanuni za mbegu tayari zimeshawaathiri wakulima wa Afrika ya Kusini[11], na kuwafanya wawe tengemezi, kuharibu udongo, na kujipa uhakika wa masoko kwa wale wanaouza mbegu za makampuni[12]. Kwa nchi nyingine kama vile Uganda na Tanzania, kanuni hizi za kuhusu mbegu zimepitishwa hivi karibuni baada ya sheria kupitishwa[13]. Sheria hizi mara nyingi hutakiwa kupitishwa na kutumika kama sehemu ya masharti ya kupata misaada kutoka kwenye nchi ambazo makampuni haya yanafanya kazi.**

**Teknolojia hizi zimekuwa zikitumika kwa ajili ya kuwatajirisha mashirika shawishi, na kuongeza ukubwa wa mabadiliko ya tabianchi kwa kusababisha hewa ya ukaa inayowadhuru wakulima wanaopambana na Haki za Mazingira.**

22 Wakati dunia inalikabili janga hili, mashirika haya yanaliona janga hili kama fursa kwao ya kutengeneza faida kubwa kubwa. Wakitegemea kuwa kutakuwa na hitaji kubwa la chakula duniani kwa miongo ijayo, biashara ya mazao ya kilimo inaelekea kuhodhi soko la dunia, na kuanzisha utamaduni wa kuwa na kilimo cha kiviwanda chenye madhara. Serikali hizo hizo zinazokutana kwenye mikutano kama ile ya COP, hukutana pia kupanga mabadiliko ya kisheria kwa nchi za kiafrika ili ziweze kunufaika na biashara ya mashirika haya makubwa. Sheria hizi zinajumuisha vifungu vinavyotamka kuwa

[10] Grain 2015: *Land and Seed Laws Under Attack: Who is Pushing Changes in Africa?* https://bit.ly/2GpQhkG

[11] African Center for Biodiversity 2017: *Seed Capture in South Africa: A Threat to See Freedom, But Seed Movements Fight Back.* https://bit.ly/2InvIY9

[12] African Center for Biodiversity 2017: *Harmonised Corporate Seed Laws in Africa: Where does this leave smallhold farmers?* https://bit.ly/2q1IQ8q

[13] African Center for Biodiversity, 2016: *Changing Seed and Plant Variety Protection Laws in Tanzania.* https://bit.ly/2pVQzW7

[14] Group of Twenty

vitendo vya wakulima wadogo kuwa ni vya kijinai, kama vile kuhifadhi na kupeana mbegu. Kwa kupitia umoja wa usalama wa chakula na lishe, nchi kumi za Kiafrika ikiwemo Msumbiji zitatakiwa kubadilisha sheria zao ili ziweze kupata misaada ya kifedha kutoka kwa wafadhili wa kundi la G8 (sasa ni G20[14]). Mara nyingi sera za aina hii zinaweka kipaumbele cha faida kwa mashirika haya na kuwanyima wananchi na dunia tuliyomo ustawi wa kimaisha kwasababu makundi hayo yanafungwa kwenye mikataba ya kimataifa. Mashirika yenye nguvu yanayotawala teknolojia zinazotumika kwenye kilimo cha kiviwanda huzishawishi serikali kupokea msaada wa kisheria na kifedha kwa ajili ya kushinikiza matumizi ya teknolojia hizi kwa wakulima wadogo duniani kote.

Kuenea huku kwa kilimo cha kiviwanda kunaathiri moja kwa moja jithada za Kilimo cha Kiekolojia katika kuhakikisha kuwa kuna Haki ya Mazingira. Biashara ya mazao ya kilimo inadai kuwa peke yake inaweza kutatua tatizo la mabadiliko ya tabianchi na kukabiliana na janga la uhaba wa chakula kwa njia ya uharibifu. Lakini ni aina





## Kilimo cha Kiekolojia cha wakulima wadogo

**Kinaendana Uoto wa asili**

Kinazingatia na kuelewa kuwa upo uhusiano wa viumbe kwa viumbe na mazingira yao.

**Kinathamini ekolojia na bayoanuwai**

Ni kilimo cha kuchanganya mazao yenye sifa tofauti. Kinazingatia mazao yenye mifumo tofauti ya mizizi kwa ajili ya kuunganisha udongo na kuukinga udongo usimomonyoke. Ni kilimo kinachohifadhi maji.

**Mchanganyiko:** Kulinda bayoanuwai na uhimilifu wa mifumo ya ekolojia. Kilimo cha mazao mchanganyiko. Upatikanaji wa mazao mengi yenye aina tofauti za lishe, uhuru wa chakula.

**Uzalishaji kwa ajili ya matumizi ya jamii husika**

Kiwango kidogo na cha kati.

**Kuhudumia Udongo**

Mbolea za kioganiki – huongeza uhai wa udongo, rutuba inayotokana na mazao ya shambani. Udhibiti wa wadudu kwa njia za asili – huhifadhi uhai wa udongo.

Kulinda udongo kwa vizazi vijavyo.

**Uhuru wa Mbegu**

Haki za wakulima kujiamulia kuhusu mbegu.

Kubadilishana na kutunza mbegu.

**Gharama ndogo za pembejeo**

Rutuba iliyoko shambani inajiongeza yenyewe. Hakitegemei mazao ya mashirika makubwa. Matumizi makubwa ya nguvu kazi – kwasababu ya uhitaji wa ufuatiliaji wa karibu wa matumizi ya ardhi. Ufanisi katika matumizi ya nishati.

**Masoko ya ndani**

Kilimo hiki kinalenga zaidi kuzalisha chakula kinachoendana na utamaduni wa eneo husika. Kinategemea sana mtandao wa masoko ya ndani na kufupisha umbali kati ya wazalishaji na walaji, na hivyo kupunguza umbali wa kusafirisha chakula.

## Kilimo cha Kiviwanda

**Kinaharibu Uasilia**
Kinatumia kwa kiasi kikubwa cha uoto wa asili kwa malengo ya kuyapatia faida mashirika makubwa.

**Ni kilimo cha zao moja**
Kinasisitiza sana ulimaji wa zao moj. Kinakuwa katika hatari kubwa ya mlipo wa wadudu waharibifu wa mazao. Momonyoko wa udongo. Kinahitaji matumizi makubwa ya umwagiliaji.

**Mfanano:** Kupotea kwa ekolojia ya kilimo na uharibifu wa mifumo ya ekolojia. Ni kilimo kinacholenga masoko. Hakuna uhakika wa chakula chenye lishe bora, hivyo kuwa na hatari ya utapiamlo.

**Kinacholenga mnyororo wa usambazaji wa kidunia**
Kilimo cha kiwango kikubwa.

**Kunyonya Udongo**
Matumizi ya mbolea za kemikali – huharibu uwezo wa udongo kukaa na rutuba. Viuatilifu vyenye sumu – huua vijidudu rafiki na wadudu wengine pia. Na vina madhara kwa afya ya binadamu. Hatari kubwa ya kutokea mafuriko, mmomonyoko wa udongo, na maporomoko ya udongo. Gharama kubwa za kuagiza pembejeo. Hudhoofisha udongo, na kuvuruga mustakabali wa vizazi vijavyo.

**Utegemezi wa Mbegu**
Mbegu zinamilikiwa na makampuni makubwa ya biashaya kilimo.
Sheria zinazowafanya wakulima wadogo wawe na makosa ya jinai wanapotumia mbinu zao za kilimo.

**Gharama kubwa za pembejeo**
Mashirika yanatengeneza faida. Nishati nyingi hutumika – wakulima wadogo wanahamishwa maeneo yao. Ni kilimo kinachohitaji sana nishati ya mafuta ya petroli.

**Masoko ya Kimataifa**
Kinalenga uzalishaji wa bidhaa za chakula
Kinalenga zaidi kuzalisha kwa ajili ya masoko ya kimataifa. Kuna minyororo mirefu ya usambazaji wa chakula.

hii hii ya kilimo ndiyo iliyosababisha majanga haya, na inaendelea kuwaathiri wakulima wadogo kwa kuwaweka kwenye madeni, utegemezi wa kununua mbegu, mbolea, na viuatilifu ambavyo vinamilikiwa na kuzalishwa kwa kiwango kikubwa na mashirika hayo. Ni aina hii ya kilimo inayoyafanya mashirika haya kukua na kuwa wenye nguvu sana kwenye mfumo wa uzalishaji wa chakula duniani kwa kuhalalisha uporaji wa ardhi, na kupuuza maarifa ya asili.

Misingi ya madai ya biashara ya mazao ya kilimo imejikita katika hoja ya kuondoa masuala ya haki za mazingira yasiwepo katika uelewa wetu wa mabadiliko ya tabianchi. Kwa maneno mengine, kudai kuwa suluhisho za janga hili ni za kiufundi (zile za mapinduzi ya kijani) na siyo za kisiasa (zinazoelezwa kwenye Haki za Mazingira). Hivyo, kwa kuuza biadhaa zao wanajiona wao ndio wamiliki wa suluhisho za janga la mabadiliko ya tabianchi, wanazishawishi serikali kuhimiza kilimo cha kiviwanda kwa wakulima wadogo. Kwa kuwaingiza wakulima wadogo katika masuala haya ya kilimo cha kibiashara, wanawabana wabaki katika udhibiti wa biashara ya kilimo kwa kuamuriwa mazao ya kulima kwa ajili ya chakula. Hii inamaanisha kuwa wanapuuza na kuondoa matumizi ya maarifa ya asili.



Katika mazingira mengi, masimulizi kuhusu janga hili yamekuwa yakitumika kuhalalisha uporaji wa ardhi au kupora rasilimali. Hoja kuwa ardhi lazima itumike ipasavyo inajikita katika madai kuwa wakulima wadogo hawawezi kutumia vizuri ardhi kwa shughuli za kilimo. Kwa njia hii, mashirika yanayohusika na biashara ya kilimo husababisha migogoro na kupora maeneo ya vijijini yanayokaliwa na wakulima wadogo, kubadilisha mazingira asilia na kuwa mashamba makubwa ya mazao kwa ajili ya kuuza nje, kufanyia biashara dunia yetu, na kunyonya rasilimali zilizopo na kuziondoa mikononi kwa jamii zinazozunguka na kuziweka kwenye umiliki wa makampuni yenye ushawishi. Hatua ya kwanza ni kupambana kwa ajili ya Haki za Mazingira kwa ajili ya kupinga suluhisho hizo potofu. Watu na mazingira asilia lazima viwe kipaumbele katika mfumo wa uzalishaji chakula.

## *Kisanduku cha 4: Uporaji wa ardhi: Majangwa ya Kijani Msumbiji*

*Hapa tunajadili namna uzalishaji wa miti ya eucalyptus kama zao la biashara ulivyosababisha uporaji mkubwa wa ardhi. Lakini inaweza kuwa ni zao la pamba, tumbaku, au zao lolote la kutengenezea mafuta. Bado tunajiuliza swali dogo: je ardhi inadibidi iwe kwa ajili ya uhusiano wa karibu kati ya mazingira asilia, kuleta chakula, na kuwapa wakulima wadogo uhakika wa maisha? Au je ni kinyume chake, kwamba ardhi inapaswa kuwa ni rasilimali ya kujitafutia faida kubwa, kuwa chanzo cha pesa kwa makampuni madogo yanayotumia mbinu za kilimo cha kiviwanda? Kwa vyovyote, kwa maslahi ya Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo na Haki za Mazingira, swali lililotangulia mwanzo ndio la muhimu.*

**Unapopita kwa gari katika eneo la Chimoio mkoa wa Manica nchini Msumbiji, haiwezekani upite bila kuona uwanda wa mashamba makubwa ya miti ya eucalyptus iliyopandwa kwa mistari iliyonyooka vizuri kabisa kama vile ni mistari ya askari wanajeshi waliosimama kwa nidhamu ya hali ya juu. Mapema kabla ya kupita kwenye mashamba hayo ya miti tulipita shamba kubwa la miparachichi lililozungushiwa uzio huku likilindwa na walinzi wenye silaha wanaofuatilia watu wanaoingia. Mwanakijiji na mwanachama wa Kikundi cha Wakulima Wadogo kiitwacho UNAC anatuonyesha shamba la eucalyptus wakati tunaendelea na safari, akisema[15],**

**"Hicho ndo tunachoita Jangwa la Kijani".**

**Mmiliki wa shamba hilo kubwa la eucalyptus ni kampuni ya kireno inayoitwa Portucel Soporcel Group, ambayo hivi karibuni imebadilishwa jina na kuitwa** *The Navigator Company***. Katika mkoa huu, kuna matukio mengi ya uporaji wa ardhi**



[15] Masimulizi haya yametoka kwenye utafiti wa pamoja kati ya Afrika Kontakt, UNAC, ZIMSOFF na LVC SEAf.

yasiyozungumziwa. Tuliambiwa na wajumbe wa chama cha wakulima kinachoitwa 3 De Fevereiro kwamba kampuni hiyo huwalaghai wakulima wadogo ili waachie ardhi yao kwa kuwapa ajira kwenye shamba hilo kubwa, kutoa fidia kwa mashamba yao, na wakati mwingine wanaahidiwa kujengewa shule na hospitali. Wakishapata maeneo wanayotaka, wakulima wadogo hao wanakuja kugundua baadaye kuwa kumbe zilikuwa ahadi tupu, nao kujikuta hawana ardhi na kazi pia hawana. Kampuni inageuza ardhi iliyokuwa ikitumika na wakulima wadogo kujipatia chakula na kuwa Jangwa la Kijani ili wapate hela kutokana na kuuza karatasi nje. Wakati mwingine huchukua ardhi bila haya ya kuwasiliana na wakulima wadogo. Wanatumia mwanya wa kuona kuwa wakulima wengi wadogo wa eneo hilo hawana hati za umiliki wa mashamba yao, wanaenda moja kwa moja serikalini wakiwa na madai kuwa ardhi ya eneo husika imepoteza rutuba na haifai kwa kilimo na hakuna anayeitumia. Halafu wanalipa serikalini ili wapewe ardhi hiyo, na kuwafukuza wakulima wadogo baada ya kupewa hati za umiliki wa eneo husika. Huu ni mfano halisi wa uporaji wa ardhi.



Mashamba makubwa yana lengo moja tu, nalo ni kutengeneza fedha kwa ajili ya makampuni shawishi. Karatasi inapelekwa katika masoko ya kimataifa, uzalishaji wake unatumia nishati kubwa na kutoa hewa chafu angani, na hivyo kukuza mabadiliko ya tabianchi. Zaidi ya hayo, ardhi iliyokuwa na mchanganyiko wa uoto wa asilia halafu baadaye ikageuzwa kwa ajili ya kilimo cha zao moja tu, ardhi yake huharibika na mfumo wa ekolojia huvurugika na hivyo kushindwa kunyonya hewa ya kaboni dayoksaidi (CO2). Wakulima wadogo wanajikuta hawana ardhi ya kilimo, hawana urithi wao, na hawana kipato cha kuwawezesha kuishi, na hivyo idadi ya wanaoathirika na tamaa ya mashirika haya inaongezeka. Mapambano ya Haki za Mazingira pia ni mapambano dhidi ya uporaji wa ardhi, mchakato wa kuiba ardhi ya wakulima wadogo na kuigeuza chanzo cha mapato ya makampuni shawishi.

**Kwa maelezo zaidi:**

*A Land Grab for Pulp* **https://bit.ly/2GQd7Sx**

*Newsletter Julho 2017* **https://bit.ly/2GQpmKT**

*Como Resistir as Empresas de plantacoes de arvores?* **https://bit.ly/2EEyT66**

*The G8 and land grabs in Africa* **https://bit.ly/2GU09iW**

*The land grabbers of the Nacala Corridor* **https://bit.ly/24R2D8N**

*Um Hectare, Uma Chapa de Zinco* **https://bit.ly/2EH7mRm**

# Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima wadogo kinafanikisha Haki za Mazingira



Wakulima sehemu nyingi duniani wanapambana na mabadiliko ya tabianchi, na mfumo wa uzalishaji unaosababisha janga hili ambao unatakiwa kudhibitiwa ni ule wa uzalishaji chakula. Vuguvugu la Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo na lile la Uhuru wa Chakula yanalenga kukabiliana na nguvu za ushawishi za makampuni makubwa yanayohodhi rasilimali za kilimo kama vile mbegu, mbolea, ardhi na maji. Inapaswa msingi wa uzalishaji wa chakula uwe ni kwa watu, na siyo mashirika makubwa ya kimataifa. Watu ndio wanaojua thamani ya ardhi yao, wanaitumia kwa ubunifu, na wanapeana maarifa hayo wao kwa wao. Hao ni wakulima wadogo wenye uwezo wa kuilisha dunia nzima, na kutuliza mabadiliko ya tabianchi, na ni walaji wanaostahili kupata chakula chenye lishe bora na chenye afya na kinachoendana na utamaduni wao. Kwa kujali masuala yanayohusu utamaduni wa chakula unaothamini watu wote na dunia nzima, Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo ni jambo la kwanza na ni hatua ya muhimu kabisa katika kupigania Haki za Mazingira.

Kilimo cha Kiekolojia kinawaweka huru wazalishaji na walaji dhidi ya mfumo wa uzalishaji unaohatarisha tabianchi na kunyimwa nyenzo zao za kukabiliana na tatizo hilo. Njia za kilimo cha Mapinduzi ya Kijani huwalazimisha wakulima kuchukua mikopo mikubwa na kuzalisha chakula kwa ajili ya kuuza nje na uzalishaji huo hauwi rafiki kwa mazingira. Kwa ajili ya kupambana na hali hiyo, wananchi wa ngazi za chini wanapigania Haki za Mazingira.

Makampuni yanayofanya biashara ya kilimo huhimiza matumizi ya kiwango kikubwa cha nishati kwa ajili ya kupata mazao mengi ya kukidhi mahitaji ya soko la kimataifa bila ya kujali madhara yanayotokea kwenye udongo na madhara kwa dunia. Wanahimiza kutumia suluhisho potofu za kukabiliana mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kulinda masoko na kuuza bidhaa zao kuliko kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa kufanya hivyo, wanapuuza, kukandamiza na hata kupoteza maarifa ya asili, ambayo ni muhimu sana katika mapambano dhidi ya haki za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo ambako mabadiliko ya





tabianchi yanaendelea kujitokeza. Ni maarifa haya ya asili, na siyo kusisitiza matumizi ya maarifa ya kutoka mbali yanayopatikana kwenye mikutano ya mazingira (COP) na maarifa haya ya asili ndiyo yahimizwe kutumika katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Kadiri athari za mabadiliko ya tabianchi zinavyoongezeka na kuwa na madhara makubwa zaidi, biashara ya kilimo inasisitiza ubinafsishaji na kilimo cha mashamba makubwa ya mazao ya biashara ambayo yanaathika zaidi na mabadiliko ya tabianchi pamoja na majanga mengine kama vile ukame na mafuriko. Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo hupambana na haya yote kwa kufanya kinyume chake; yaani kupanda mazao mbalimbali yanayoendana na mazingira husika, na kusimamia kwa nguvu zote haki za kijadi za matumizi na umiliki wa ardhi. Kwa njia ya sheria za haki miliki, ambazo zinakubaliwa na serikali kwenye majadiliano ya kibiashara, mashirika yanayojishugulisha na biashara ya kilimo yanajaribu kuangamiza kabisa mifumo ya kupeana mbegu na mifumo ya wakulima wadogo na badala yake wanaweka mifumo ambapo wakulima watakuwa tegemezi kwenye bidhaa zinazouzwa na makampuni haya. Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kinahimiza matumizi ya njia hizi za asili kama vile kubadilishana mbegu, matumizi ya nishati kwa kiwango kidogo na uhifadhi wa rutuba kwenye mashamba wakati wa kilimo, mambo ambayo yanawasaidia wakulima kujaribisha mazao yanayohimili ukame na kuimarisha udongo.

Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kinahitaji sera za serikali zisizozuia njia za asili za uzalishaji, na ili kufanikiwa katika hilo kunahitajika mapambano. Mapambano haya ni kwa ajili ya Haki za Mazingira. Maamuzi kuhusu namna serikali za mitaa zinasimamiwa na nani azisimamie, lazima yafanyike ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kuulisha ulimwengu. Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo ni siasa, na ni maisha yanayotakiwa kupiganiwa.

# Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo ni kwa ajili ya kila mtu

Tofauti na kilimo cha kiviwanda ambacho kinawalenga wachache, Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo ni jumuishi, na kiko kwa ajili ya kila mtu. Kinatoa pia nafasi kwa makundi yaliyo hatarini na yanayokandamizwa kuwa na haki ya kupaza sauti zao. Wanawake wana nafasi ya kipekee katika mfumo wa kidunia wa uzalishaji chakula, kwakuwa wao ndio wazalishaji wakubwa wa chakula, wakiwa kwa wingi wao na kama walinzi wa bayoanuwai na mbegu za kilimo[16]. Kwa kuzingatia athari mbaya za mfumo wetu wa kuzalisha chakula kwa tabianchi, nafasi ya wanawake na wasichana imekuwa hatarini zaidi kutokana na mfumo dume ulio kandamizi unaowapa amri badala ya wao kuwa sehemu ya uzalishaji.  Kwa vile wana majukumu mengi ya kuendesha familia zao kwa kutafuta nishati ya kupikia na kuchota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kuhakikisha ustawi wa watoto na wazee kwenye nyumba, wanawake wamefanywa kuwa tegemezi sana wa mazingira asilia yanayowazunguka. Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri misimu ya mvua na hivyo kuathiri pia upatikanaji wa maji kwani yanakuwa adimu na yanakuwa mbali na makazi ya watu, na mazao yanahitaji huduma zaidi ili yaweze kukua. Hali hii huwalazimisha wanawake (na watoto) kutembea umbali mrefu kutafuta maji na kuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, na hilo huongeza ugumu wa wao kupata mazao katika kipindi chote cha mwaka, hasa kwakuwa hawawezi kutegemea tena misimu ya mvua iliyozoeleka.



Wanawake wamekuwa waathiriwa wa mfumo uliopo sasa, ambao unaendelea kuwafanya wasitambulike kwenye jamii. Wanawake wanakabiliana na ukatili wa kimfumo (uchumi, ajira, mazingira, kimwili, kingono na kisaikolojia), huku matukio ya mauaji ya

[16] Nyéléni 2007: *Women's declaration on food sovereignty* https://nyeleni.org/spip.php?article310

wanawake yakiongezeka[17]. Uliberali mamboleo na mfumo dume vinashirikiana na vimechangia kwa kiasi kikubwa ukandamizaji na ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana walioko maeneo ya vijijini, na pamoja na kutengeneza mazingira ya kuwafanya wanawake na wasichana washindwe kujiamini na kuwasabishia mazingira dhaifu ya kazi...na wakiwa kwenye mazingira yanayosababisha mabadiliko ya tabianchi na hivyo kushusha thamani na utu wao[18].

Mfumo dume wa kibepari umehamia pia kwenye kilimo cha kiviwanda, ambapo wanawake wamekuwa waathiriwa wakubwa wa ukandamizaji. Kwa Afrika, wanawake hawana uwezo wa kumiliki ardhi, na hivyo hawawezi kuwa na rasilimali zozote zile na kushindwa kujiamulia kuhusu maisha yao na miili yao. Mbali na ukweli kuwa wanawake ndio nguvu kazi kubwa na ndio wanaoongeza thamani ya mazao ya chakula na ulaji, wametengwa katika kufanya maamuzi kwenye sera za umma hadi kwenye maamuzi yanayohusu matumizi ya fedha za familia, na kwa sehemu kubwa wanathiriwa zaidi na utapiamlo. Mara nyingi wanaume ndio wamekuwa waamuzi wa masuala yote ya kwenye kaya, kama vile mazao gani yapandwe, ni mazao gani yauzwe, na mazao gani yakuwekwa ghalani, na namna ya kutumia kipato kilichopatikana baada ya mauzo. Zaidi ya hayo, kilimo cha kiviwanda na masoko ya kimataifa vinategemeana, na hali hii husababisha tatizo la mfumo dume, ukosefu wa haki za kijinsia na ukatili.



Ingawa Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo hakiwezi kuushinda mfumo dume uliopo, kwa kiasi kikubwa unaweza kukabiliana na sheria kandamizi za mfumo dume. Ni kilimo kinachoweza kubadilisha maisha ya wanawake kwasababu majukumu yao yanatambuliwa na kuonekana kwa njia za kilimo wanazotumia. Sasa hivi kidogo kidogo wanawake wameanza kuhusishwa kwenye maamuzi katika ngazi tofauti kuanzia kwenye

[17] LVC 2017. Declaration - V Women's Assembly.
[18] LVC 2014. Manifesto - IV Women's Assembly of La Via Campesina.

vuguvugu na kwenye mashirika mbalimbali. Kwa mfano, maamuzi yaliyofanyika kwenye mifumo ya kiutawala (kama vile LVC na mashirika wanachama). Ingawa kuna mafanikio haya, bado kuna kauli za kimfumo dume zinaendelea kuwepo, hasa kuhusiana na majukumu yanayoonekana ni ya kijinsia zaidi na maamuzi kwenye ngazi ya kaya, ambako mfumo dume bado unaonekana umekita mizizi. Hili mara nyingi hutegemea sana na mazingira ya kiutamaduni (katika jamii na kwenye ngazi ya kaya) ambako Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kinafanyika, na kutegemea ni kwa kiasi gani jamii na njia za usawa wa kijinsia zinatumika kuandaa dira, mikakati na mbinu za kufanya kazi. Hiki kinaendelea kuwa kikwazo kwa Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kama nyenzo ya kupambana na kushinda mfumo dume.

Masuala mengine yanayohusiana na mfumo dume, kwa kiasi fulani, yameondolewa. Kutokana na gharama kidogo za Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo, wanawake wanaweza kwa kiasi kikubwa kushiriki na kunufaika na mazao mengi na kilimo mchanganyiko. Kwa kulima mazao mchanganyiko kunakoimarisha mfumo wa ekolojia, kubadilishana ujuzi, wanawake wanaweza kusimamia kwa mafanikio masuala ya kilimo cha chakula na kupata chakula cha kutosheleza mahitaji ya lishe kwa ajili yao wenyewe na kwa kaya zao. Kupungua kwa utegemezi wa wanawake kwa wanaume kwenye Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kutasaidia kuleta uwiano wa madaraka, ambapo wanawake watakuwa na nafasi ya kushiriki katika majukumu na madaraka, kulingana na uzito wa majukumu yenyewe. Wakati kilimo cha kiviwanda kikiwa kimeshindwa kutatua changamoto zinazowakabili wanawake na masuala ya usawa wa kijinsi, Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kimeonyesha kuwa kinaweza kutatua matatizo yao. Kwa mara nyingine tena ni vema kusisitiza kuwa Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo hakihusiani na kanuni fulani, bali ni mfumo halisi wa maisha. Ni mfumo halisi wa maisha ambao ni jumuishi, na ambapo si kwamba mwanaume anajitwalia tu mamlaka kwasababu ni mwanaume bali anapewa mamlaka pale

tu atakapoonekana anastahili kuwa nayo. Mabadiliko ya tabianchi ni janga la kisiasa, kijamii, na kiekolojia ambalo litaendelea kuwa kubwa endapo sauti za wakulima wadogo (na za walaji pia), hasa wanawake, zitaendelea kunyamazishwa au kupuuzwa. Ndio maana mapambano kwa ajili ya Haki za Mazingira lazima yaende sambamba mahusiano mazuri ya kijinsia.

Kitendo cha wanaume kwenye familia kuhamia mijini au kwenye nchi nyingine kwa ajili ya kutafuta maisha bora, pamoja na vifo vyao, kufungwa au kuuawa na viongozi wa kisiasa wa nchi husika, kunawafanya wanawake kuwa katika hali ngumu zaidi. Wameelewa na mzigo wa majukumu ya kutoa huduma ya chakula kwa familia zao, kuwahudumia watoto – ambao wamekuwa katika tishio la ukatili wa kingono, vifo na kutengwa – huku wakiendelea kutetea maeneo yao na miili yao dhidi ya vitendo vya udhalilishaji vinavyofanywa na watu wenye nguvu[19].

Vijana wanakandamizwa na mfumo dume. Kwa upande wa Afrika ya Kusini mwa Jangwa la Sahara, vijana huyakimbia maeneo yao kwasababu ya vita, mabadiliko ya tabianchi na hali ngumu za kiuchumi na kijamii. Uporaji wa ardhi unaofanya na makampuni ya kimataifa kwa ajili ya uwekezaji wa kwenye nishati, uchimbaji wa madini na maendeleo ni jambo la kawaida sana. Nguvu kazi ya vijana kwenye kazi hizo haithaminiwi na wananyonywa sana[20].



Ardhi na maeneo ya kilimo vimefanywa bidhaa, na unyonyaji unaofanywa na makampuni kwa kisingizio cha uwekezaji na uporaji wa ardhi vimewafanya vijana kukosa ardhi, hasa wasichana. Kwa wakati huo huo, tija kidogo kwenye kilimo na mazingira magumu vinawafanya vijana kushindwa kufanikiwa kimaisha kupitia ardhi. Hali hii inakuwa ngumu zaidi kutokana na mabadiliko ya tabianchi[21].

[19] LVC 2017. Declaration - V Women's Assembly.
[20] VII International Conference: Youth Assembly Declaration
[21] VII International Conference: Youth Assembly Declaration

Ili kuondoa kabisa mfumo dume na ubaguzi popote ulipo, vijana lazima wajitoe kwa kufanya kazi kubwa ya kujitathmini na kuchunguza mambo yanayoendekeza mfumo dume na ubaguzi wa rangi[22].

Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo ni njia ya kuwa na uhuru wa chakula na suluhisho kwa janga hili kubwa la kidunia linahosu sekta nyingi pamoja. Ni maono ya kisiasa, mfumo wa maisha na chanzo cha maarifa kutoka kwa mababu zetu. Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kimekuwa nyenzo ya kuunganisha pamoja uzoefu mbalimbali duniani. Kwa mfano, mbinu ya mkulima mdogo-kwa-mkulima mdogo (campesino-to-campesino) imekuwa yenye mafanikio na nyenzo muhimu ya kubadilishana taarifa na kuimarisha mawasiliano na mafunzo. Mbinu hii inaheshimu sana ujuzi asilia wa maeneo na wati wake, na kwa njia hii maarifa hayo yanaweza kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine[23].



Vijana pia wanawakilisha daraja kati ya jamii za mijini na vijijini. Ingaw ahali huonekana tofauti, baadhi ya aina za ubaguzi wa kimfumo ambazo makundi hukabiliana nazo ni matokeo ya nguvu kandamizi za mashirika ya kimataifa yenye mtaji mkubwa na nguvu za ushawishi. Vijana duniani kote wamekuwa wakikusanyika na kufanya kilimo cha mijini, kurejea kwenye kilimo, kujenga jamii imara kwa ajili ya uhuru wa chakula au kufanya kazi ya kutetea haki za kijamii kwa namna yoyote ile[24].

Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo na Haki za Mazingira ni kwa ajili ya kila mmoja.

[22] VII International Conference: Youth Assembly Declaration
[23] VII International Conference: Youth Assembly Declaration
[24] VII International Conference: Youth Assembly Declaration



## “Dunia ni Mama Yetu”

Mfumo wa kuzalisha chakula kwa njia ya kilimo cha kiviwanda ni njia ya kuhodhi na kutawala maisha kwenye dunia kwa lengo la kuwatajirisha mashirika shawishi ambayo ni ya wachache. Wale wenye mamlaka wanapuuza majanga kama vile mafuriko, ukame, udongo usio na rutuba, mabilioni ya watu wanaoshinda njaa, na dalili chache za kuangamia kwa mazingira asilia yanayotuweka duniani. Ni jambo gumu kuficha madhara haya yanayoangamiza na kuwalazimisha wasio na hatia kubeba msalaba. Mfumo wa uzalishaji chakula unaharibu udongo, misitu, uoto wa asili, uwanda, bahari, mito, na maziwa, na kuongeza mabadiliko ya tabianchi, na kuwafanya watu waishio vijijini kuwa na maisha ya kitumwa. Ni mfumo wa uzalishaji unaosababisha kifo, ukandamizaji na ukatili.

Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo ni mfumo bora wa maisha. Ni mfumo wa maisha unaotambua kuwa Dunia ni mama

yetu. Umejengwa na watu wote kwa pamoja na jamii husika zinazungumza lugha moja ya uhifadhi wa mazingira asilia na kuweza kuishi uelewa huo kwa kujali mazingira hayo asilia. Ni kilimo kinachojenga na kuimarisha mifomo ya ekolojia, kunyonya hewa ya kaboni, na kuhimiza ustawi wa bayoanuwai. Kinawakomboa wote walioko vijijini ambao wamelazimika kubadilisha mfumo wao wa maisha na kuharibu mazingira. Kilimo cha Kiekolojia cha Wakulima Wadogo kinaona ardhi kama kitu kitakatifu, na kuna uhusiano mtakatifu kati ya watu na ardhi yao. Mbegu, udongo, maji, hewa, siyo vitu vya kujipatia faida bali ni rasilimali za kusaidia maisha yaendelee kuwepo duniani.

Mabadiliko ya tabianchi ni tishio kubwa kwa uhai wa mwanadamu. Ni jambo la kupaswa kuelewa kuwa siyo rahisi kwa watu kujiona wako tofauti na mazingira yao, sisi ni sehemu ya mazingira hayo, nguvu ya mazingira ni kubwa sana. Hii inaonyesha kuw ipo haja kubwa ya kufanya mageuzi makubwa. Jambo pekee la kufanya ni kwa mfumo wa uzalishaji wa chakula kutoendelea kutoa hewa chafu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea sasa. Na ili tuweze kufanya hilo, tunapaswa kujielekeza kwenye jamii za wakulima wadogo, wanawake vijijini, na wote walioko pembezoni, ambao tayari wana mbadala wa maisha. Tunatakiwa kujifunza kwa wale ambao tayari wanaishi kwa kuheshimu mazingira yao asilia, kwa gharama yoyote ile. Kwa wale wanaotegemea maisha yao kupitia mfumo wa uzalishaji chakula na jamii zao, na wana ujuzi wa namna ya kuzalisha kwa ajili ya dunia nzima, wajue kuwa watu wa ulimwengu huu wanahitaji mazingira wanayoharibu, na ni kwa njia ya Haki ya Mazingira tutaweza kufanikiwa katika hilo.

*Photography by Camillo Springborg & Jon Nelson*
*Layout by Francesca Desmarais*
*Fist icon by Christopher T. Howlett*

LA VÍA CAMPESINA

*Afrique australe et Orientale*

AFRIKA KONTAKT